

MPANGO WA MUNGU KWA KULIJENGA KANISA NA KUFIKIA WALIOPOTEA

Mungu alikiwa na mipango ya kanisa kabla misingi wa dunia (waefeso 1:4). Mungu alijua jinsi Kanisa litakuwa na wokovu kwa waliopotea. Alifunua mipango zake kwa wanafunzi wake mara ya kwanza na wakafuata hizo mipango kwanzia siku ya pentekoste baada ya kufufuka kwa Yesu kutoka wafu. (Matendo ya mitume 2:1-47)

Wakristo wa kwanza walifuata mpangilio wa mungu vile walivyo onye ashwa, Na kanisa lilioanza pale yerusalemu. Mara tu, likapanika yudea kwa haraka, samaria, na kwa ulimwenguni yote.

Kwa sasa tukifuata mipango hizi, injili itaendelea ,kanisa litakuwa na nafsi zita okolewa. (1 Petro 1:18-20, 1 Wakorintho 2:7, 2 Timotheo 1:9, Tito 1:2)

Maandiko ya Kimsingi: Matthew 28:18-20, Marko 16:15-16, Luka 24:44-47

1. "Enendeni"- Jukumu letu kama wakristo ni kufundisha ukweli.

a.) 1 Wakorintho 1:19-20 – Ni lazima tufuate mpango wa mungu na hekima zake.

b.) Matendo 8:4 – Ni lazima twende kila mahali tukihubiri / kufundisha neno.

c.) 1 Timotheo 4:16 – Ni lazima tujue mafundisho, tuishi mafundisho na tufundishe mafundisho.

d.) 2 Timotheo 4:2 – Hubiri /fundisha neno hata kama litapokelewa vizuri ama kukataliwa.

2. "Katika Ulimwengu Wote" – Nilazima tuelewe ya kwamba ulimwengu wote umepotea:

a.) Waefeso 4: 17-19 – Wengi ulimwenguni hawajui hali yao.

b.) Yohana 3: 16-18 – Kristo alikuja kwa wote kwa sababu wote wamepotea.

c.) Matendo 1: 6-8 – Tuhubiri kwa ulimwengu kwa sababu wote wamepotea.

d.) Matendo 8: 1-5 – Lazima twende kila sehemu.

3. "Kila Kiumbe" – Wanadamu Wote. Kila Mtu.

a.) Warumi 1:16 – Injili ni ya mataifa yote na watu.

b.) Matendo 10: 34-35 – Mungu hana upendeleo kwa mtu – kila taifa.

c.) Matendo 15: 11 – Kupitia neema ya Mungu wote wanaweza kuokolewa.

d.) Yakobo 2:1, 5 – Hana heshima kwa watu.

e.) 1 Wakorintho 1: 26-29 – Mara nyingi wale tunafikiria ni wanafunzi wazuri sio hao.

4. " Yeye anaye amini na kubatizwa ata okolewa. – inahitaji zote.

a.) Matendo 2:37-41,47 – Mahubiri ya kwanza yalihubiriwa yote pamoja na toba.

b.) Matendo 8: 12, 36-38 – Walipo amini walibatizwa.

c.) Matendo 10: 47-48 – Wayahudi/ Mataifa iliamuliwa wabatizwe.

d.) Matendo 16: 14-15 – Wakwanza katika Philippi wakabatizwa waipo amini.

e.) Matendo 16: 31-34 – Askari jela alibatizwa alipo amini.

f.) Matendo 18:8 – Wengi wa korintho waliamini na kubatizwa walipo skia.

- g.) Matendo 19:1-5 – Wale waaliofundishwa kupitia yohana mbatizaji wakiamini walibatizwa kwa Kristo.
- h.) Matendo 22:16 – Sauli alipokua amefundishwa alibatizwa ili kuoshwa dhambi zake.
5. **“Wafundishe Kutii na kufuata kila kitu ambacho kimeamuriwa” – Ni lazima kumtii Kristo.**
- Waebrania 5:8-9 – Kristo ni mkombozi kwa wale wanao mtii.
 - Matendo 4:11-12 – Wokovu ni kupitia Kristo pekee. (Yohana 14:6)
 - Matendo 5:29 – Tunahitajika kumtii Mungu badala ya mwanadamu.
 - Matendo 20:26-27 – Ni lazima tutangaze na kutii mashauri ya Bwana.
 - Timotheo 2:15 – Nilazima tusome ili kujua ambavyo tunastahili kutazama na kutii.
 - 2 Timotheo 3: 14, 4:4 – Bibia yote iliandikwa kwa mashauri na mwelekezo wa Mungu.
 - Jude 2 – Ni lazima tuhudumie Imani.

Kanisa la kwanza, Wakristo wa kwanza,

Kuchukua injili ya Kristo – Wakolosi (1:23) ulimwenguni katika kizazi kimoja kwa muda usiozidi miaka 70 , Bila vijikaratasi via kuchapishwa, edio, Televisheni na Mtandao.


Vilichochea na upendo wa mungu; upendo wa kweli, na upendo kwa walio potea, ili kufanya makusanyiko ya makanisa ya Kristo, kwa miji mikuu na halikadhalika vijiji vidogo vidogo na kwenye maduka.

Jinsi gani tunaweza kufanya sasa, tukiwa na rasilimali ya kisasa au teknolojia ya kisasa, na kusafiri kwa hali ya juu?


Inahitajika na sisi tuwe na upendo wa kujitolea kwa waliopotea na kulijenga kanisa. Ukweli wa neema ya mungu, wokovu na kanisa ni kupata kujua ukweli.

Sisi kama waumini wa kanisa la kristo tunawapenda.

Leo umejifunza Kuhusu mpango wa mungu wa kulijenga kanisa na kufikia walio potea kupitia kijikaratasi hiki.



MPANGO WA MUNGU KWA KULIJENGA KANISA NA KUTUMIKIA WALIOPOTEA



Kimetafsiriwa na
Evangelist Olao Kennedy Odanga
KENYA – EAST AFRICA